UAMBIKAJI KAMA DHANA KUU:

TOFAUTI YA UAMBISHAJI NA UNYAMBULISHAJI

Na

Sebastian Nyerere Mbwillow

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam @January 2017

Maneno ya lugha asilia ya binadamu huundwa kwa njia mbalimbali. Uundwaji huo wa maneno hufanywa ili kuweza kukidhi matakwa ya kimawasiliano na hata kuiendeleza lugha husika. Miongoni mwa njia hizo za uundaji wa maneno ni kama vile njia ya uradidi, kubuni, uambatanishaji, uambatizi kwa maana ya uambishaji na unyambulishaji kwa kutaja chache. Njia hizi, pamoja na nyinginezo, zimetumika na zinaendelea kutumika sana katika kuitajirisha lugha kimsamiati. Wanaisimu na hasa wanamofolojia wamekuwa katika mjadala kwa muda mrefu, hasa wakijadili mambo kama, ni njia gani inazalisha maneno mengi kuliko nyingine? Ipi inafaa kuwa ndiyo njia mahususi? Nini ubora na udhaifu kwa kila njia? Na mengine mengi.

Fasili nyingi zimetolewa kuhusiana na hizi za uambishaji na unyambulishaji. *Kamusi Sanifu ya Kiswahili* inafasili dhana hizo kama ifuatavyo;

> *"unyambulishaji ni uambatanishaji wa viambishi kwenye mzizi ili kujenga neno"*
> *"uambishaji ni utaratibu wa kuambatisha viambishi kwenye mziziz"*
> TUKI (2013)

Maelezo hayo ya ufafanuzi huu uliotolewa na TUKI (2013) yanakinzana. Hayaoneshi waziwazi kuwa hizo ni dhana mbili tofauti. Maelezo haya yanataka kutueleza kuwa hakunana utofauti kati ya unyambulisha na uambishaji.

Gawasike (2016) anadai kuwa mkanganyiko huu ni wa muda mrefu. Anadai wataalamu kama Nkwera (1978), TUKI (1990), Rubanza (1996), wamefanyia kazi dhana hizo tokea awali. Lakini bado mpaka sasa zinachanganywa.

Rubanza (1996) anaona kuwa unyambulishaji ndiyo dhana kuu iliyogawanyika katika sehemu tatu: Uambikaji, Mzizi na Unyambuaji ikiwa katika mtindo wa ungoe. Anafafanua kwa kutumia kielelezo hapo chini

kielelezo 1.



Chanzo ni Gawasike (2016)

Kwa kielelezo 1. ni wazi kuwa mwanamofolojia yeyote anaweza kusema kuwa, unyambulishaji ndiyo dhana kuu. Ambapo chini yake kuna uambikaji, mzizi na unyambuaji. Pia yaweza kuelezwa zaidi kuwa uambikaji ni upachikaji wa viambishi kabla ya mzizi na unyambuaji ni upachikaji wa viambishi baada ya mzizi. Lakini je wataaalamu wengine wana kubaliana na kielelezo hiki?

Massamba (2004) anadai kuwa unyambulishaji, na anaufananisha dhana ya *derivation* katka lugha Kiingereza kuwa ni utaratibu wa kupachika viambishi kwenye mzizi ili kuunda maneno mapya. Anatolea mfano ufuatao;

a) $\text{Zuia}_{T} > \text{vizuio}_{N}$
b) $\text{Pima}_{T} > \text{kipimo}_{N}$
c) $\text{Kula}_{T} > \text{chakula}_{N}$ (*chanzo Massamba 2004)*

Maelezo haya ni wazi kuwa, kwanza upachikaji hauangalii kuhala. Yaani ama ni kabla au baada ya mzizi. Pili ni wazi kuwa mtaalamu huyu amechukua dhana ya unyambulishaji kutoka lugha ya Kiingereza na kuiingiza kwenye Kiswahili kama ilivyo bila kuzingatia utofauti wa sheria na kanuni za kila lugha. Massamba (2004) anafasili dhana ya uambishaji (*affixation*) kuwa ni taaluma ya mofolojia inayohusu utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, katikati au baada ya mzizi. Anabainisha kuwa kuna aina mbili za uambishaji: uambishaji nyambulishi (*Derivation*) na uambishaji kisarufi (*inflection*).

Yawezekana kuwa utata mkubwa unaletwa kwa kuanza kuzitumia dhana za Kiingerezaza *affixation*, *derivation* na *inflection.* Hii ni kutokana na ukweli kuwa, dhana hizi katika lugha hiyo zimejadiliwa kwa kina na wataalamu mbalimbali kiasi kwamba kwa lugha yao hakuna uvulivuli au mkamnganyiko mkubwa kama uliopo katika lugha yetu ya Kiswahili.

Mtajuka (2012) anajaribu kutafsiri dhana hizo tatu kuwa ni: *Affix* ni kiambishi, *derivation* ni mnyambuliko au unyambulishaji na *inflect* ni nyambulisha. Inasisitizwa hapa kuwa kuna haja ya kufanyiwa utafiti na kuwa na mjadala wa kutosha kabla ya kuhamishia dhana hizi katika Kiswahili. Hapa swali moja mtu analoweza kujiuliza haraka haraka ni, je kuna tofauti gani kati ya *inflection, derivation* na *affixation* za Massamba (2004) na Mtajuka (2012)?

O'grad na wenzake (1997) wanazielezea dhana hizo wakidai kuwa *affixation* (uambishaji-kama aliviita Massamba) ni kitendo cha kuongeza viambishi kwenye mzizi. Wanazidi kueleza kuwa uambishaji huo waweza kuwa kabla, ndani au baada ya mzizi. *Derivation* (unyambulishaji-Massamba, na mnyambuliko au unyambulishaji-Mtajuka) kuwa huhusu uundaji wa neno lenye maana na au la kategoria tofauti na lile la awali lilotokana nalo kwa njia ya upachikaji wa viambishi. Kwa kutumia mfano ufuatao wanaonesha jinsi *derivation* inavyotokea na kudhihirika waziwazi.

	Kiingereza		**Unyambulishaji**	
a)	Sell	"uza"	sell-er	"muuzaji"
b)	Write	"andika"	writ-er	"mwandishi"
c)	Sing	"imba"	sing-er	"muimbaji"

O,grad na wenzake (wamesha tajwa) wnadai kuwa *inflection na derivation*, vyote hivi ni matokeo ya *affixation.* Maelezo haya yanashadadia kuwa katika lugha hiyo walau kuna uangavu kwa kiasi kikubwa kuhusu dhana hizo.

Katamba na Stanham (2006) wakiwa wanajadili juu ya mofimu wanadai kuwa mofimu zinaweza kugawa katika makundi makuu mawili kwa kutumia kigezo cha kikazi. Makundi hayo mawili yatakayopatikana ni *Derivation* (unyambulishaji kwa mujibu wa Massamba) na *Iflection* (mnyambulisho kwa mujibu wa Mtajuka). Wanadai zote hizo ni njia za uzalishaji maneno, na kwamba zinaunda maneno kwa njia tofauti. Wanadai kuwa:

> *"Derivation morpheme form new word either:*
> *i) By changing the meaning of the base to which they are attached. Eg.kind →unkind = both are adjective but with opposite meaning.*
> *ii) By changing the word class. Eg. Kind (Adj) →kindly (Adv).*
> *iii) By causing a shift in the grammatical subclass of a word without moving it into a new word-class. Eg. Friend →friendship. Both are noun.*

Inflection morphemes do not change referential or cognitive meaning. They modify the form of a word so that it can fit into a particular syntactic slot. Inflections mark plural, persons, tense, comparative degree and superlative.

Mofimu nyambulishi inaunda neno jipya ama;

i) Kwa kubadili maana ya shina ambalo imepachikwa. Mf. karimu →utokarimu = yote haya ni Vivumishi vya maana kinyume.

ii) Kwa kubadiri kategoria ya neno. Mf. Karimu (V) →kiukarimu (E)

iii) Kwa kusababisha kuhama kundi mahusi ndani ya aina hiyo hiyo ya kategoria ya neno husika pasi na kuhama na kuunda neno jipya. Mf. Rafiki → urafiki. Yote ni nomino.

Mofimu za mnyambuliko zenyewe hazibadili kategoria ya neno wala maana ya msingi. Myambuliko huonesha uwingi, nafsi, njeo, na ulinganisho.

*(*Tafsiri ni yangu).

Maelezo haya ya Katamba na mwenzake (wameshatajwa), yanathibitisha kuwa katika lugha hiyo dhana hizo hazina utata mkubwa. Pili ni ushahidi kuwa katika lugha yetu bado hatuna visawe madhubuti vinavyoweza kusawili vile vya Kiingereza (*inflection, derivation* na *affixation*). Na hivyo kuvirejelea ni kuzidi kujichanganya na kufanya dhana hizi zisieleweke zaidi. Tatu ni kengele miongoni mwetu wanamofolojia kuwa tufanye mjadala wa kutosha ili kupunguza mkanganyiko huu.

Kwa sababu hii basi namuunga mkono Gawasike (2016) anayependekeza kuwa kuwe na dhana tatu: uambikaji iwe ndiyo dhana jumuishi ambapo ndani yake kupatikane dhana hizo mbili yaani uambishaji na unyambulishaji. Kielezo namba 2. Kinaonesha namna Gawasike (keshatajwa) anavyopendekeza.



kielelezo 2.

Chanzo Gawasike (2016)

Kwa mujibu wa Gawasike anapendekeza kuwa mzizi uwe ndiyo msingi wa mgawanyo. Pia anashauri kuwa badala ya kutumia dhana ya mofimu, itumike mofu au viambishi. Yaani badala ya kusema ni kitendo cha upachikaji mofimu baada au kabla ya mzizi, tuseme ni kitendo cha upachikaji wa mofu au viambishi. Anadai zaidi kuwa mofimu ni dhana telezi mno.

Uambikaji ni kitendo cha upachikaji au uongezaji wa mofu au viambishi kabla au baada ya mzizi wa neno, kiini au shina la neno. Uambikaji ni njia muhimu sana katika uundaji wa maneno. Uundaji huo wa maneno hutokea baada ya kuwa vimeongezwa viambishi kabla, baada au kabla na baada ya mzizi. Kinachosisitizwa hapa ni kuwa njia ya uundaji wa maneno iwe ni uambikaji. Na uambishaji na unyambulishaji ziwe ni aina za uambikaji ambapo tofauti yake kuu iwe ni pahala pa upachikaji. Yaani iwe inasemwa kuwa, viambishi vyote vitakavyotokea au pachikwa kabla ya mzizi viingie kwenye uambikaji. Na vile vya baada ya mzizi viinngie kwenye unyambulishaji. Kitu kingine ni kuwa michakato yote hiyo (uambishaji na unyambulishaji) inaweza kubadili maana, kategoria na au kutanua maana na kufanya kazi za kisarufi. Kwa mfano

i) {-som-} **mzizi** {soma} **shina**
ii) Som-a
iii) Som-o
iv) Som-e-w-a
v) A-na-soma
vi) M-li-wa-soma
vii) Ma-som-o
viii) M-soma-ji

Kwa kutumia mfano (i) – (viii) ni vema ikaeleweka kuwa (i) ni mzizi wa neno na shina, ambapo maneno yote yaani (ii) – (viii) yametokana nao. Namba (ii) – (iv) viambishi vimepachikwa baada ya mzizi. Namba (v) – (vi) viambishi vimepachikwa kabla ya shina. Kisha namba (vii) – (viii) viambishi vimepachikwa kabla na baada ya mzizi na shina.

Kwa hiyo, itakuwa ni rahisi kuzifafanua dhana hizo zilizokuwa na uvuli vuli tena hata kwa kutumia maneno machache kabisa. Kuwa uambishaji ni upachikaji wa mofu/viambishi kabla ya mzizi au shina. Unyambulishaji ni mchakato wa upachikaji wa mofu/viambishi baada ya mzizi wa neno au shina. Na uambikaji ni mchakato wa kimofolojia unaohusu kupachika viambishi/mofu kabla, baada na au kabla na baada ya mzizi au shina la neno. Upachikaji wa viambishi kabla ya mzizi/shina huitwa uambishaji, na upachikaji wa viambishi baada ya mzizi/shina huitwa unyambulishaji.

Baada ya kutolewa ufafanuzi kuhusu dhana za unyambulishaji, uambishaji na uambikaji, yafaa sasa kujadili ufanano na utofauti uliopo kati ya uambishaji na unyambulishaji. Hebu kwa kuanza tuchuguze kwa mifano kuona ni kwa namna gani dhana hizi zinafanana.

Unyambulishaji na uambishaji zote zatokana na dhana kuu ya uundaji maneno ya uambikaji kamailivyojadiliwa hapo juu. Katika kueleweka hapa kielelezo kifuatacho ni muhimu kutumika.



Kielelezo 3.

Uambishaji na unyambulishaji zote zaweza kuunda neno jipya. Kwa kutumia mfano hapo chini (i) – (iv) inadhihirisha ya kuwa, waweza kunyambulisha neno kitenzi (katika (i) – (ii)) na kuunda nomino ambayo ni neno jipya kwa kutumia viambishi vinominishi. Katika (iii) – (iv) inadhihirisha ya kuwa kuna uwezekano maneno ambayo awali yalikuwa ni vivumishi baada ya uambishaji kinominishi {u-} yamebadilika na kuwa nomino.

i) Som-a → som-o
ii) Chez-a → chez-o
iii) Zuri → u-zuri
iv) Bora → u-bora

Uambishaji na unyambulishaji zote zinahusu kuambika viambishi. Yaani uambishaji huitwa hivyo, kwa kuwa kuna mchakato wa kupachika au kuambika viambishi, hali kadharika na unyamburishaji pia. Hivyo basi yaweza kusemwa kuwa viambishi ndiyo nguzo kubwa na tegemeo la uwepo wa michakato hiyo. Kwa lugha nyepesi ni sawa na kusema bila viambishi hakuna uambishaji wala unyambulishaji.

i)	A-na-soma	viambishi {a-, -na-}
ii)	Tu-li-u-cheza	viambishi {tu-, -li-, -u-}
iii)	Som-e-w-a	viambishi {-e-, -w-, -a}
iv)	Som-esh-a	viambishi {-esh-, -a}

Uambishaji na unyambulishaji zote zaweza kutobadili kategolia ya neno bali zikatanua maana ya neno husika. Neno husika lililoambikwa likabaki ndani ya kategoria ile ile. Tuchunguze mfano huu wa neno *soma* ambalo lipo katika kategoria ya kitenzi.

Uambishaji a-na-ni-soma

a- Kiambishi awali upatanisho wa kisarufi na nafsi ya tatu umoja mtenda.

-na- kiambishi awali njeo iliyopo

-ni- kiambishi awali kirejeshi cha mtendwa

-soma ni shina.

Unyambulishaji som-e-w-a

-e- kiambishi tamati kauli ya kutendea

-w- kiambishi tamati kauli ya kutendwa

-a kiambishi tamati maana.

Sasa tuchunguze kutofautiana kwa dhana hizi mbili baada ya kuwa tumejadili ufanano wake. Hapa ni vema kusisitiza kuwa unyambulishaji na uambishaji ni dhana mbili tofauti. Ni tofauti kwa kuwa kama isingalikuwa tofauti basi tungekubaliana na O'buchi na Mukhwana (2015) na habwe na Karanja (2004) katika kauli zao hapo chini.

> *"uambishaji ni utaratibu wa kuongeza viambishi kwenye mzizi ili kulipa neno husika maana mahususi (uk.111). unyambulishaji, hapa maneno ya kategoria mpya huweza kuundwa kwa kuongeza viambishi kwenye maneno au mizizi ya maneno Fulani.*
>
> *O'buchi na wenzake (2015)*
>
> *"uambishaji ni utaratibu wa kuongeza viambishi katika mofimu mzizi wa neno. Unyambulishaji ni utaratibu katika lugha wa kupachika au kuongezea viambishi kwenye mzizi wa neno ili kuunda maneno mapya.*
>
> *Habwe na Karanja (2004)*

Kwa maelezo ya wataalamu hawa ni kuwa unyambulishaji na uambishaji ni sawa. Kwa maana kwamba zote ni uongezaji wa viambishi iwe kabla au baada au kabla na baada. Tofauti yao ni

kuwa likizaliwa neno jipya basi iwe umeongeza viambishi kabla au baada mchakato huo utaitwa unyambulishaji.

Kama ambavyo imekwisha kujadiliwa hapo juu kuhusu ufanano wa unyambulishaji na umnyumbulishaji, pia zipo tofauti ambazo kwazo ndiko kulikopelekea zikawa ni dhana mbili tofauti. Tofauti kubwa ipo katika sehemu ambako mchakato huo unatokea na dhima yake.

Tofauti ya kwanza ni sehemu ya utokeajia wa mchakato wenyewe. Kama ambavyo tumekwisha kuona, uambishaji hutokea kabla ya mzizi au shina la neno. Inasisitizwa sehemu ni kabla ya mzizi wa neno kama inavyooneshwa hapo chini.

i) A-na-ni-cheka
ii) A-na-ku-sema
iii) A-li-m-saidia

Wakati unyambulishaji hutokea baada ya mzizi au shina. Kinachosisitizwa hapa ni baada ya mzizi/shina. Kwa msingi huu bila kujali matokeo ya uongezaji/upachikaji wa mofu/viambishi, uambikaji ukifanyika baada ya mzizi huo utaitwa unyambulishaji. Chunguza mfano ufuatao unavyoshadadia dai hili.

i) Som-o
ii) Som-e-an-a
iii) Som-w-a

Tofauti nyingine ni katika kazi ya viambisha vya mchakato husika. Viambishi vingi vya uambishaji hufanya kazi za kuonesha nafsi, mtendwa au mtenda, njeo na upatanisho wa kisarufi. Kazi hizi haziwezi kuoneshwa katika unyambulishaji. Hata kama kiambishi kile kile kilichotokea katika uambishaji kitatokea kwenye unyambulishaji kitafanya kazi tofauti. Chunguza mfano huu.

i) A-na-ni-tamani
a-nafsi,umoja na upatanisho wa kisarufi
-na- njeo
-ni- mtendwa
-tamani shina la neno *ananitamani.*

Vivyo hivyo unyambulishaji pamoja na mengine hudokeza kauli mbali mbali. Jambo hili haliwezi kutokea kwenye uambishaji. Katika lugha ya Kiswahili vitenzi ndivyo hudokeza dhana ya kauli. Kauli hizo huweza kuwa kauli ya kutenda, kutendeka, kutendewa, kutendeana, kwa kutaja chache. Tuone mfano.

i) Lim-i-a *kauli ya kutendea*
ii) Lim-w-a *kauli ya kutendwa*
iii) Lim-ik-a *kauli ya kutendeka*
iv) Lim-i-an-a *kauli ya kutendeana*

Unyambulishaji na uambishaji katika lugha ya Kiswahili hautokei katika kila neno au kategoria ya maneno ya Kiswahili. Kwa mfano ni rahisi kuambisha takribani katika vitenzi vyote vya Kiswahili, lakini inakuwa vigumu katika nomino nyingi. Tuone mfano ufuatao.

i) Nyumba $_{N}$ → nyumba-ni $_{E}$
ii) Uwanja $_{N}$ → uwanja-ni $_{E}$
iii) Juma $_{N}$ → *Juma-ni
iv) Njombe $_{N}$ → *ma-njombe
**muundo usiosahihi.*

Kwa hakika si kila nomino inakubali uambishaji au unyambulishaji, majina hasa majina ya kipekee baadhi hayakubali kuambikwa. Hili linaweza kuwa moja ya tatizo la uambikaji kama njia ya uundaji wa maneno ya Kiswahili. Pamoja na hivyo uambikaji ni njia ambayo inamsaada mkubwa katika kuongeza msamiati wa lugha na kupanua maana ili kukidhi mahitaji ya kimawasiliano.

Marejeo

Gawasike, A. (2016) “Dhana ya Uambikaji katika Kiswahili”, imesomwa 17-11-2016 saa 9:24 jion. http://www.academia.edu/8511140/

Habwe, J na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Phonix Publishers. Nairobi.

Katamba, F. Na Stanham, J. (2006) *Morphology*: Toleo la Pili. Palgrave Macmillian. London.

Kihore, Y. M,nawenzake (2003). *SarufiMaumboya Kiswahili Sanifu*. TaasisiyaUchunguziwa Kiswahili, Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B, (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Taasisi yaUchunguziwa Kiswahili, Dar es Salaam.

Mtajuka, Khamis A. (2012). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili-Kiarabu,* TATAKI. Dar essalaam.

O’buchi, S. na Mukhwana (2015). Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele. The Jomo Kenyata Foundation. Kenya.

O'Grady, W. na wenzake (1996). *Contemporary Linguistics*. Pearson Education Ltd. United Kingdom

Rubanza, Y. I, (1996). *Mofolojiaya Kiswahili.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam